



وَمَنْ أَنْهَا اللَّهُ أَرْبَعَةِ أَيَّارٍ مَّا مَنَّا بِهِنْكُمْ وَعَلَى الْعَصْلَى لَدُنْهُ لَتَسْتَفْلِئُنَّهُ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَفَلَ  
الَّذِي كَمَا قَلِيلُهُمْ وَلَيُكَثِّنَنَّهُمْ وَلَيُنَاهِيَنَّهُمْ أَرْبَعَةِ أَيَّارٍ مَّمَّا لَيَعْلَمُهُمْ مِّنْ بَعْدِ حِفْظِهِمْ أَمْنًا  
يَعْبُدُونَهُ لَا يُشْرِكُونَ بِهِ شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ

Toleo: 1446 / 07

Jumatatu, 28 Jumada II 1446 H

30/12/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**  
**Uchumi wa Kibepari Unasambaratisha Familia na Misingi yake**  
**(Imetafsiriwa)**

Warsha ya karibuni ya kinachoitwa ‘usawa wa kijinsia’ iliyo fanyika ndani Ngorongoro, Kaskazini mwa Tanzania iliibua suala la uwepo baadhi ya wanandoa kutoka katika jamii za wafugaji ambao wametelekezwa na waume zao walioondoka vijiji ni kwenda mijini kutafuta kazi, na wakati mwengine waume hao hawarudi katika familia zao.

Hali hiyo si tu imewapelekea wanandoa hao (wanawake) walioachwa vijiji ni upweke, taharuki, huzuni na kukata tamaa, bali pia inawalizimisha wanawake hao kubeba majukumu mazito ya kutunza familia majumbani mwao, wakiwa na msaada mdogo kutoka jamii zao. (The Guardian, 27 December 2024)

Kuhusiana na jambo hilo Hizb ut Tahrir Tanzania ina haya ya kusema:

Mbali na uwepo wa taathira za tamaduni za kikabila ambazo hatuwezi kuzipuuza kuwa na kijishehemu kidogo kuhusiana na jambo hilo. Bali sababu msingi ni sera za uchumi wa kibepari ambazo zimepelekea yafuatayo:

1. Kuwepo unyonyaji wa kiuchumi kwa kisingizio cha uwekezaji wa kigeni uliopelekea msingi wa kiuchumi katika vijiji kusambaratika na kubwagika, kwa kuwa nyenzo nyeti za kimaisha kama maeneo ya kulisha mifugo, vyanzo vya maji kama mito hubinafsishwa. Mgogoro wa Mbuga ya Ngorongoro ni mfano hai wa hilo: <https://hizb-ut-tahrir.info/en/index.php/2017-01-28-14-59-33/news-comment/22692.htm>

2. Maumbile ya mfumo wa kibepari kukosa udhati katika kuwatumikia raia, hivyo nguvu kubwa ya kihuduma hutumiwa kwa kipimo cha kimaslahi, kiasi cha mfumo huo kushughulika zaidi na maeneo ya mijini, kinyume na maeneo ya vijiji ambayo hutelekezwa na kukoseshwa huduma muhimu. Matokeo ya jambo hilo ni kuibuka wimbi kubwa la uhamiaji kutoka vijiji ni kwenda mijini. Kuwafanya watu wa vijiji kukimbilia mijini kutafuta hali bora.

Hali hizo huwalazimisha watu wa vijiji kutafuta namna nyengine ya kujikimu maisha yao.

Kadhia hii ni miongoni mwa matunda machungu ya mfumo wa kibepari. Hali inayopaswa kuwa amsha wanafikra wakiwemo wanaharakati wa kinachoitwa ‘usawa wa kijinsia’ ambao badala ya kubeba kauli mbiu za kiuwongo za ‘kuinua hali ya wanawake’ na ‘haki sawa’ ambazo huvuruga zaidi nidhamu ya kijamii, wangepaswa wawekeze juhudii zao kuondoa moja kwa moja mfumo wa kibepari kwa mbadala wa mfumo mwengine ambao ni Uislamu.

Mfumo huo wa Uislamu una uwezo wa kukabiliana na matatizo yote ya wanadamu kwa uadilifu na katika msingi wake.

**Masoud Msellem**  
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**  
**Hizb ut Tahrir Tanzania**